TANGAZO LA SERIKALI Na. 499 la Tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimeandaliwa chini ya kifungu cha 427)*

KANUNI ZA TARATIBU ZA UINGIAJI KATIKA MAENEO FUNGWA ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA MAENEO FUNGWA

4. Watu ambao majukumu yamebainishwa.
5. Milango ya maeneo fungwa.
6. Kuingia kwenye maeneo fungwa.
7. Mazoezi ya utayari.
8. Vifaa vya upimaji.
9. Misamaha.

SEHEMU YA TATU
MAKOSA NA ADHABU

10. Makosa na adhabu.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

11. Uzuiaji.
12. Tathmini na utoaji wa taarifa.
13. Ushughulikiaji wa malalamiko.

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,

(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 427)*

## KANUNI ZA TARATIBU ZA UINGIAJI KATIKA MAENEO FUNGWA ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitakulikana kama Kanuni za Taratibu za Uingiaji Katika Maeneo Fungwa za Mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika kwa meli za Tanzania, popote zilipo na meli nyingine zikiwa ndani ya maji ya Tanzania.

(2) Bila kuathiri ujumla wa kanuni ndogo ya (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa-

(a) chombo cha starehe;
(b) meli ambayo haina nahodha, mfanyakazi na mlinzi;
(c) meli ya kivita au msaidizi wa majini;
(d) meli inayomilikiwa au kuendeshwa na Serikali kwa huduma zisizo za kibiashara; na
(e) vyombo visivyopungua urefu wa mita 24 au tani 50 za jumla.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii "chombo cha starehe" maana yake ni chombo ambacho kimsingi hutumika kwa michezo au burudani.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi-

"eneo fungwa" maana yake ni eneo ambalo halijaundwa

kukaliwa na mfanyakazi mfululizo na ina mojawapo au sifa zote zifuatazo:
(a) nafasi ndogo za kuingia na kutoka; na
(b) isiyoingiza hewa ya kutosha;

"Kanuni" maana yake ni Kanuni ya Ufanyaji Kazi kwa Vitendo za Mabaharia Wanaosafiri Majini Toleo la 2015 kama ilivyorekebishwa mwaka 2022;

"meli ya kubeba gesi" maana yake ni meli iliyotengenezwa au kubadilishwa kwa ajili ya kubeba gesi iliyoyeyushwa kwa wingi au bidhaa nyingine zilizoorodheshwa katika Jedwali la Sura ya 19 ya Kanuni za Kimataifa za Ujenzi na Vifaa vya Meli Zinazobeba Gesi Zilizoyeyushwa kwa Wingi au kwa kifupi chake kinachojulikana kama "Kanuni za IGC";

"meli ya mafuta" maana yake ni meli yoyote iliyotengenezwa au kubadilishwa kwa ajili ya kubeba mafuta au kemikali kwa wingi;

"meli ya Tanzania" maana yake ni meli iliyosajiliwa au kupewa leseni chini ya masharti ya Sheria katika bandari ya Jamhuri ya Muungano;

Sura ya 415 "Msajili" maana yake ni Msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"mwajiri", kuhusiana na meli, maana yake ni mtu ambaye kwa wakati huo anamwajiri baharia;

"nahodha" inajumuisha mtu yeyote isipokuwa rubani mwenye amri au msimamizi wa meli, ndege ya baharini au chombo kingine kinapokua juu au karibu na maji;

"Notisi ya Usafiri Majini" maana yake ni Notisi ya Usafiri Majini iliyotolewa na Msajili;

Sura ya 165 "Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafiri Majini;

Sura ya 415 "Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"tani" maana yake ni tani za jumla, na tani za jumla za meli yenye tani mbadala zitachukuliwa kuwa kubwa zaidi ya tani hizo; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya usafiri majini.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA MAENEO FUNGWA

Watu ambao majukumu yamebainishwa

4.-(1) Itakuwa ni wajibu kwa kila mwajiri kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, isipokuwa pale ambapo wajibu huo utabainishwa kwa mtu mwingine yeyote.

(2) Endapo sharti lolote la Kanuni hizi limetoa jukumu kwa mtu asiye na mamlaka na jambo husika kwa sababu hana wajibu katika uendeshaji wa meli, jukumu hilo litakuwa pia kwa mtu yeyote mwenye mamlaka na jambo hilo.

Milango ya maeneo fungwa

5. Nahodha wa meli atahakikisha kwamba milango yote ya maeneo fungwa yasiyotumika kwenye meli yanafungwa au vinginevyo yamezuiwa kuingiwa, isipokua kama ni muhimu kuingia humo.

Kuingia kwenye maeneo fungwa

6.-(1) Mmiliki wa meli, mwajiri na mtu mwingine yeyote aliyerejewa chini ya kanuni ya 5 atahakikisha kwamba-

(a) mifumo ya kazi zilizowekwa na zinazotumika melini, kuhusiana na afya na usalama kazini, inajumuisha mifumo ya kuingia na kufanya kazi katika maeneo fungwa; na
(b) tathmini za vihatarishi vya kuingia na kufanya kazi katika maeneo fungwa zinafanyika.

(2) Nahodha atahakikisha kwamba mifumo ya kazi iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1)(a) inazingatiwa ndani ya meli.

(3) Mtu hataingia au kubaki katika eneo fungwa, isipokuwa kwa mujibu wa mifumo ya kazi iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1)(a).

(4) Mmiliki wa meli, mwajiri na mtu mwingine yeyote aliyerejewa chini ya kanuni ya 5, katika kutekeleza majukumu yao chini ya kanuni hii, atazingatia kikamilifu kanuni na miongozo iliyomo kwenye Sura ya 10 ya

Kanuni.

Mazoezi ya utayari

7.-(1) Nahodha atahakikisha kwamba mabaharia ambao majukumu yao yanajumuisha kuingia au kuokoa kutoka kwenye maeneo fungwa melini, wanashiriki kwenye mazoezi ya utayari yanayozingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3).

(2) Mazoezi ya utayari yaliyoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) yatarekodiwa kwenye kitabu rasmi cha kumbukumbu.

(3) Mazoezi ya utayari-

(a) yatafanyika melini kwa kipindi kisichozidi miezi miwili;

(b) yatapangwa na kufanyika katika hali ya usalama, kwa kuzingatia mwongozo katika Sura ya 15 ya Kanuni;

(c) ni pamoja na-

(i) ukaguzi na matumizi ya-

(aa) vifaa vya kinga binafsi vinavyohitajika kuingia;

(bb) vifaa na taratibu za mawasiliano;

(cc) vifaa vilivyoainishwa chini ya kanuni ya 8;

(dd) vifaa na taratibu za uokoaji; na

(ii) mafunzo ya utoaji wa huduma ya kwanza na mbinu za uokozi.

Vifaa vya kupima

8. Katika meli ambazo zina eneo fungwa linalofikika, mmiliki wa meli na mwajiri watahakikisha kwamba-

(a) meli imebeba vifaa vinavyobebeka vya kupima hali ya hewa ambavyo vinamwezesha baharia kupima mgandamizo wowote wa oksijeni, gesi zinazolipuka au mivuke, salfidi hidrojeni na monoksidi kaboni ndani ya eneo hilo kabla baharia yeyote hajaingia katika sehemu hiyo;

(b) kifaa kilichoainishwa katika aya ya (a)-

(i) kinatunzwa katika utaratibu mzuri wa kufanya kazi; na

(ii) pale inapohitajika, kinatengenezwa mara kwa mara na kupimwa kulingana na mapendekezo ya mtengenezaji.

Misamaha

9.-(1) Shirika linaweza, kwa masharti itakayotoa, kutoa misamaha ya kutotumika kwa masharti ya kanuni ya 7 na 8 kwa meli binafsi au aina ya meli ambazo-

(a) ni chini ya tani 500;
(b) si meli ya SOLAS au daraja la meli za SOLAS; na
(c) zinakidhi masharti yaliyowekwa chini ya kanuni ndogo ya (2).

(2) Meli itasamehewa kutotumika kwa masharti kanuni za 7 na 8 chini ya kanuni ndogo ya (1) endapo inakidhi masharti yafuatayo:

(a) meli au daraja la meli inaendeshwa kwa mujibu wa-
    (i) ratiba inayoitaka kurudi bandarini katika kipindi kisichozidi masaa 72; na
    (ii) utaratibu ambao unahakikisha kwamba hakuna baharia melini anayeingia kwenye eneo fungwa lolote wakati meli hiyo iko baharini;
(b) hakuna ulazima wa kuzingatia masharti ya kanuni ya 7(3)(a) kutokana na-
    (i) utaratibu wa uendeshaji wa meli au daraja la meli; au
    (ii) mpangilio wa wafanyakazi melini au daraja la meli; na
(c) hakuna eneo fungwa kwenye meli au daraja la meli ambalo baharia anapaswa katika hali ya kawaida kuhitaji kuingia, isipokuwa katika mazingira ya kipekee.

(3) Endapo meli au daraja la meli limesamehewa kutotumika kwa masharti ya kanuni za 7 na 8 baada ya kukidhi masharti yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (2)(b) au (c), mmiliki wa meli na mwajiri watahakikisha kwamba-

(a) mabaharia wanashiriki katika mazoezi ya utayari sawa na yale yaliyoainishwa chini ya

kanuni ya 7(3)(b) na (c)-

(i) iwapo ni kanuni ndogo ya (3)(b), katika namna nyingine na vipindi kadri inavyoweza kutekelezeka; na

(ii) iwapo ni kanuni ndogo ya (3)(c), endapo kuingia kunahitajika katika mazingira ya kipekee, kabla ya ruhusa ya kuingia; na

(b) mazoezi ya utayari yaliyoainishwa chini ya kanuni ya 7(2), yanarekodiwa katika kitabu rasmi cha kumbukumbu.

(4) Msajili anaweza, kwa kutoa notisi, kubadili au kufuta msamaha wowote uliotolewa chini ya kanuni hii.

(5) Msamaha, mabadiliko katika msamaha au ufutaji wa msamaha uliofanyika chini ya kanuni hii-

(a) utakuwa katika maandishi;
(b) utaainisha tarehe ya kuanza kutumika; na
(c) kuhusiana na msamaha, utataja masharti, kama yapo, ambayo yametolewa.

(6) Sharti kwamba msamaha, mabadiliko katika msamaha au ufutaji wa msamaha uliotolewa chini ya kanuni hii kuwa kwa maandishi litatimia pale ambapo maudhui ya msamaha huo-

(a) yamewekwa kwa njia ya kielektroniki;
(b) yamepokelewa kwa mfumo unaosomeka; na
(c) yanafaa kutumika kwa marejeo yanayofuata.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu

10.-(1) Nahodha ambaye atashindwa kutimiza masharti yoyote ya kanuni ya 5 au 7(1) atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua dola za Marekani elfu moja au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita na kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(2) Mmiliki wa meli, mwajiri au mtu mwingine yeyote aliyeainishwa katika kanuni ya 4 ambaye atashindwa kuzingatia matakwa yoyote ya kanuni ya 6(1)

atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua dola za Marekani elfu moja au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita na kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(3) Mmiliki wa meli au mwajiri ambaye atashindwa kutimiza masharti yoyote ya kanuni ya 8 au 9(3) atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua dola za Marekani elfu moja au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita na kisichopungua miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA JUMLA

Uzuiaji

11.-(1) Meli ambayo haitazingatia masharti ya Kanuni hizi inaweza kuzuiliwa.

(2) Pale ambapo meli imezuiliwa chini ya kanuni ndogo ya (1), masharti ya kifungu cha 409 cha Sheria yatatumika, isipokuwa masharti yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (7) hayatatumika.

(3) Pale ambapo meli inapaswa kuzuiliwa chini ya kanuni hii, mtu anayeizuia meli hiyo atatoa notisi ya kuzuia kwa nahodha ambayo-

(a) inaeleza sababu za kuwekwa kizuizini; na
(b) inahitaji masharti ya notisi kuzingatiwa hadi meli itakapoachiwa na mtu yeyote aliyetajwa chini ya kifungu cha 409 (1) cha Sheria.

(4) Pale ambapo meli nyingine ambayo si ya Tanzania imezuiliwa, Shirika litaifahamisha mara moja mamlaka ya nchi ya usajili wa meli husika kwa maandishi.

(5) Pale ambapo haiwezekani kuijulisha mamlaka ya nchi ya usajili wa meli kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4), Shirika litaifahamisha ofisi ya Ubalozi wa mamlaka ya nchi iliyosajili meli, au endapo hakuna ofisi ya Ubalozi, mwakilishi wa karibu wa kidiplomasia wa nchi iliyosajili meli.

(6) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (4) na (5), "mamlaka ya usajili" kuhusiana na meli maana yake ni

Nchi ambayo meli inastahili kupeperusha bendera yake.

Tathmini na utoaji wa taarifa

12.-(1) Msajili-
(a) atafanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;
(b) atandaa taarifa inayoainisha hitimisho la tathmini; na
(c) atawasilisha taarifa kwa Waziri.

(2) Taarifa ya kwanza chini ya kanuni hii itachapishwa kabla ya mwaka wa tano wa maadhimisho wa siku ambayo Kanuni hizi zitaanza kutumika.

(3) Taarifa zinazofuata zitachapishwa kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(4) Taarifa iliyoandaliwa na kuwasilishwa chini ya kanuni hii:
(a) itaanisha malengo yanayokusudiwa kufikiwa na masharti ya udhibiti yaliyoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1)(a);
(b) itatathmini kiwango ambacho malengo hayo yanafikiwa;
(c) itatathmini endapo malengo yaliyoainishwa yana tija; na
(d) pale ambapo malengo yanatija, taarifa itatathmini kiwango ambacho yanaweza kufikiwa kwa njia nyingine inayohusisha masharti mepesi ya udhibiti.

Ushughulikiaji wa malalamiko
TS. Na. 338 ya 2018

13. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa Shirika kwa mapitio kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Wakala wa Meli Tanzania.

Dodoma,
28 Juni, 2023

MAKAME M. MBARAWA,
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*